TAARIFA YA UZALISHAJI NA UCHIMBAJI WA MAKAA YA MAWE MKOANI RUVUMA

1. UTANGULIZI

Uchimbaji na uuzaji wa makaa ya Mawe Mkoani Ruvuma ulianza mwaka 2011 kukiwa na Kampuni moja tu ambayo ni *Tancoal Energy Ltd*. Mwaka 2019 wadau wengi walijitokeza na kufanya uwekezaji katika shughuli za Makaa ya Mawe kulikopelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hayo kuanzia mwaka 2020. Uzalishaji wa Madini ya Makaa ya Mawe hutoa mchango mkubwa kwenye maduhuli yanayokusanywa na Tume ya Madini Mkoani Ruvuma. Katika kipindi cha hivi karibuni, Makaa ya Mawe yamekuwa yakihitajika sana ulimwenguni kama chanzo cha nishati na hivyo kuwa moja ya chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali. Kwa mfano, Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Ofisi ya Madini – Ruvuma ilipangiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni Kumi na Mbili (TZS 12,000,000,000.00)**. Hadi kufikia tarehe 30.06.2022, Ofisi ya Madini Ruvuma ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni ishirini na moja milioni mia tano themanini na nane laki saba na nne mia moja sabini na nne na senti arobaini na sita (TZS 21,588,704,174.46)** sawa na **Asilimia Mia Moja Sabini na Tisa (179%)** ya lengo la Mwaka huo.

Aidha, Katika Mwaka huu wa Fedha 2022/2023, Ofisi ya Madini – Ruvuma imepangiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni ishirini na sita milioni mia tatu sitini na sita laki tatu ishirini na mbili na mia sita na thelathini na senti tisini na nane (26,366,322,631.98).** Hadi kufikia tarehe **31 Disemba, 2022**, Ofisi ya Madini – Ruvuma imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni kumi na tisa, milioni mia nane hamsini na saba, laki mbili na tano elfu na kumi, na senti sitini na saba**) **(TZS 19,857,205,010.67)** sawa na asilimia **75.25** ya lengo. Katika makusanyo yote hayo, zaidi ya asilimia themanini na tano (85%) yamechangiwa na uzalishaji na uuzwaji wa makaa ya mawe. Madini haya huuzwa ndani ya nchi, nchi zinazotuzunguka, barani Ulaya na Asia kupitia bandari ya Mtwara na Dar es Salaam.

2. WACHIMBAJI WA MAKAA YA MAWE MKOANI RUVUMA

Kuna jumla ya wachimbaji Kumi na nne (14) wanaochimba Makaa ya Mawe katika Mkoa wa Ruvuma. Orodha ya Wachimbaji hao imeoneshwa katika Jedwali hapo chini.

Jedwali 1: Orodha ya wachimbaji wa madini ya Makaa ya Mawe Mkoani Ruvuma

S/No.	Parties	Commodities	Locality	Halmashauri
1	TANCOAL ENERGY LTD	Coal	Ngaka	Mbinga DC
2	RUVUMA COAL MINE LTD	Coal	Paradiso	Mbinga DC
3	MARKET INSIGHT LIMITED (MIL-COAL)	Coal	Mbuyura	Mbinga DC
4	MBUYULA COAL MINE LIMITED (BECCO)	Coal	Mbuyura	Mbinga DC

S/No.	Parties	Commodities	Locality	Halmashauri
5	GOD MWANGA GEMS LTD	Coal	Malini	Nyasa DC
6	JITEGEMEE HOLDINGS COMPANY LIMITED	Coal	Mbuyura	Mbinga DC
7	RUTANZA COAL LIMITED	Coal	Kikunja	Songea DC
8	NJUGA MINES LIMITED	Coal	Kikunja	Songea DC
9	LONGNUS ORESTUS KOMBA	Coal	Mbuyura	Mbinga DC
10	ALLY MCHEKANAE AND ISSA ALLY MCHEKANE	Coal	Mbuyura	Mbinga DC
11	DENIC MINING LTD	Coal	Mbuyula	Mbinga DC
12	ARIA COMMODITIES INTERNATIONAL LIMITED	Coal	Amani Makolo	Mbinga DC
13	TENKO LIMITED	Coal	Paradiso	Mbinga DC
14	SYNERGY INTERNATIONAL LTD	Coal	Mdunduwalo	Songea DC

3. UZALISHAJI WA MAKAA YA MAWE

Mwaka wa Fedha 2021/2022 kiasi cha Madini ya Makaa ya Mawe kilichouzwa pamoja na makusanyo yaliyopatikana kutokana na madini hayo yameoneshwa katika majedwali hapo chini.

Jedwali 2: Taarifa ya mauzo ya Madini ya Makaa ya Mawe katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2021/2022 katika Mkoa wa Ruvuma imeoneshwa kwenye Jedwali hapo chini.

Mwezi	Uzito(Tani)	Thamani(USD)	Mrabaha (USD)	Ada ya Ukaguzi (USD)
Jul-21	50,299.28	6,576,657.40	197,299.72	65,766.57
Aug-21	66,178.85	8,933,352.43	268,000.57	89,333.52
Sep-21	68,268.80	8,976,762.05	269,302.86	89,767.62
Oct-21	119,416.81	15,758,647.75	468,799.43	156,266.48
Nov-21	89,467.49	12,182,815.79	365,484.47	121,828.16
Dec-21	100,839.90	13,957,479.51	418,724.39	139,574.80
Jan-22	162,503.70	23,340,211.63	700,206.35	144,050.85
Feb-22	98,617.07	13,585,735.71	407,572.07	135,857.36
Mar-22	188,552.87	26,996,547.11	809,896.41	178,752.87
Apr-22	211,078.49	32,398,126.79	790,329.12	106,127.02
May-22	188,116.73	29,114,870.54	873,446.12	182,872.94
Jun-22	134,011.25	19,285,672.43	578,570.17	192,856.72
JUMLA	**1,477,351.24**	**211,106,879.14**	**6,147,631.69**	**1,603,054.92**

Katika mauzo hayo Jumla ya **Tani 639,482.55** ziliuzwa ndani ya nchi na **Tani 837,846.29** ziliuzwa nje ya nchi.

Jedwali 3: Taarifa ya mauzo ya Madini ya Makaa ya Mawe katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2022 hadi Disemba, 2022 katika Mkoa wa Ruvuma imeoneshwa kwenye Jedwali hapo chini

Mwezi	Uzito(Tani)	Thamani(USD)	Mrabaha (USD)	Ada ya Ukaguzi (USD)
Jul-22	239,483.39	39,440,766.46	1,069,991.36	203,006.37
Aug-22	228,861.93	35,393,035.95	908,045.78	217,821.56
Sep-22	296,470.83	48,581,259.33	1,290,289.56	209,792.29
Okt -22	318,631.25	49,572,261.12	1,316,128.67	217,704.83
Nov-22	189,393.39	27,078,724.34	655,753.18	190,183.78
Dec-22	238,533.58	36,668,618.63	935,827.04	210,761.47
Jumla	**1,511,374.37**	**236,734,665.83**	**6,176,035.59**	**1,249,270.3**

Katika mauzo hayo jumla ya **Tani 450,675.32** ziliuzwa ndani ya nchi na **Tani 1,060,699.05** ziliuzwa nje ya nchi.

4. MCHANGO WA SEKTA YA UCHIMBAJI WA MAKAA YA MAWE MKOANI RUVUMA

Kwa kipindi cha hivi karibuni Mkoa wa Ruvuma umeweza kuvutia na kupata wawekezaji wengi waliowekeza kwenye shughuli zinazohusiana na madini ya Makaa ya Mawe kama Uchimbaji, Ununuzi, Usafirishaji na Uchenjuaji.

Ufuatao ni Mchango wa madini ya Makaa ya Mawe katika Mkoa wa Ruvuma

i. Kuongezeka kwa mapato ya Serikali;
ii. Kuongeza kipato kwa mtu mmoja mmoja na kupunguza utegemezi kutokana na ajira zilizopo katika uchimbaji wa Makaa ya Mawe;
iii. Kuongeza fedha za kigeni nchini kutokana na madini hayo kuuzwa nchi za nje; na
iv. Kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri mbalimbali yatokanayo na ushuru wa huduma unaotozwa kwenye madini yanayochimbwa

5. CHANGAMOTO ZA SEKTA YA MADINI KATIKA MKOA WA RUVUMA

i. Uharibifu wa mazingira kwa kukata miti na kuharibu/kuchafua vyanzo vya maji.

ii. Kushindwa kukusanya maduhuli kutokana na kuwepo na leseni chache zinazofanya kazi. Hii inatokana na wachimbaji wadogo kutokuwa na mitaji ya kutosha kwa ajili ya shughuli za uchimbaji;

iii. Uelewa mdogo wa taarifa za kijiolojia,

6. MIKAKATI YA KUPAMBANA NA CHANGAMOTO

i. Kuendelea kuhamasisha wachimbaji kupitia chama chao kiitwacho “Ruvuma Region Miners Association” (RUVREMA) ili waweze kuomba mikopo kwa lengo la kuboresha shughuli zao;

ii. Kuendelea kutoa elimu ya Sheria ya Madini pamoja na Kanuni zake ili kuepusha migogoro katika maeneo ya uchimbaji wa madini na kupunguza kama sio kuondosha kabisa matukio ya utoroshaji na ukwepaji tozo za madini;

iii. Kuendelea kutoa elimu ya Afya, Usalama na Utunzaji wa Mazingira katika maeneo ya machimbo ili kudhibiti ueneaji wa magonjwa yakiwemo UKIMWI na magonjwa mengine ya milipuko katika maeneo ya madini; na

iv. Kuendelea kutoa huduma ya ugani kwa wachimbaji kwenye usimamizi wa utunzaji wa mazingira, kupunguza ajali na kuongeza uzalishaji kwenye uchimbaji.